Ushauri kwa Walimu Wapya

SWAHILI

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.

MKUSANYIKO WA TAARIFA ZA MWALIMU WA FAMILY DAY CARE:

Ushauri kwa Walimu Wapya

Baada ya kuamua kwamba unataka kuwa mwalimu wa Family Day Care na kujisajili na huduma ya Family Day Care, ni muhimu kuanza vizuri. Ushauri huu umekusanywa na walimu wengine na unajumuisha mambo ambayo yaliwasaidia wakati wao wenyewe walikuwa wanaanza.

Ushauri kuhusu jinsi ya kutengeneza mazingira ya watoto yaliyo salama, yenye kibali na ya kuelimisha

- Hakikisha unafahamu ni watoto wangapi ambao unakubalika kisheria kuwatunza na kuwaelimisha katika wakati wowote, (hadi watoto saba, na kusiwe zaidi ya wanne walio chini ya umri wa shule – wakiwemo watoto wako walio chini ya miaka 13).
- Tekeleza mpangilio wa shughuli kwa mujibu wa Utaratibu wa Mafunzo ya Miaka ya Awali (Early Years Learning Framework). Utaratibu huo umetafsiriwa kwa baadhi ya lugha zingine mbali na Kiingereza – Tafuta "Early Years Learning Framework translated" kwenye Google.
- Panga nyumba yako vizuri. Hakikisha watoto wanaweza kufikia vitu wanavyovihitaji (k.m. kofia na vitu vya kuchezea) na hawawezi kufikia vitu ambavyo hawapaswi kushika.
- Kuwa na vifaa unavyohitaji (viti vidogo vya watoto, meza ya kubadilishia mtoto nepi, vitanda vya kawaida na vya watoto wadogo) ili kurahisisha mambo.
- Kuwa na zana zinazofaa, lakini zisiwe nyingi kupita kiasi (k.m. vifaa vya kuchezea vya kujenga, vifaa vya sanaa na ufundi, ala za muziki, vifaa vya kutumia wakati wa kuigiza michezo ya kubuni).
- Fuata sera za huduma yako ili kuhakikisha unawapa watoto pahali salama na panaposisimua.
- Nenda kwenye kikundi cha michezo au shughuli yoyote inayotolewa na huduma yako.
- Iwapo una matatizo yoyote, fahamisha huduma yako mapema.

Ushauri wa jinsi ya kuendesha biashara

- Weka rekodi nzuri na sahihi na uhakikishe familia zinatia saini KILA WAKATI wanapoleta mtoto wao na wanapokuja kumchukua.
- Katu usitie saini chochote ambacho hauelewi.
- Hakikisha kuwa unajua sera na utaratibu wa huduma yako kuhusu ada na rekodi za mahudhurio.
- Hakikisha una bima sahihi ya Family Day Care na umjulishe mtoa bima wa nyumba yako kuwa unaendesha huduma za Family Day Care nyumbani mwako.
- Shiriki katika masomo ya kujiendeleza kitaaluma kwa jinsi unavyoweza. Hii itakusaidia kuendesha biashara yako kwa utaalam zaidi na utazifanya familia kujihisi tulivu zaidi wanapokuachia mtoto wao.
- Hakikisha unafanya majukumu ya usimamizi unapoendelea kutoa huduma. Usiache majukumu yote yarundikane ili uyafanye mara moja.
- Kuwa na urafiki na walimu wengi iwezekanavyo. Watakuwa rasilimali yako ya kuuliza maswali.

IWAPO UNA WASIWASI WOWOTE, ULIZA HUDUMA YAKO!

Huduma ya Family Day Care ambayo umejisajili nayo inapaswa kukusaidia kujitayarisha kuwa mwalimu. Wanapaswa kukupa mafunzo ya usajili na kukusaidia kuelewa sheria ambazo ni lazima ufuate. Wanaposwa kukusaidia kutayarisha usimamizi unaohitaji. Wanaweza kuwa na miongozo na vijitabu vya maelekezo vya kukusaidia kuelewa kinachohitajika.

Ushauri kuhusu kufuata sheria

- Kila wakati fuata sheria za huduma kuhusu mambo kama vile kurekodi mahudhurio, usiri na malalamiko.
- Iwapo unashuku kuwa jambo fulani si halali au haliruhusiwi, uliza. Ukihisi kuwa huwezi kuzungumza na huduma yako, wasiliana na mamlaka ya udhibiti ya jimbo lako (ikiwa ni kuhusu usalama wa mtoto au elimu) kwa **www.acecqa.gov.au** au Idara ya Elimu na Mafunzo ya Serikali ya Australia kwa nambari **1800 664 231**, ikiwa ni kuhusu mitindo ya utozaji ada.
- Rekodi saa sahihi za utunzaji.
- Jifunze kuhusu Kanuni za Kitaifa za Huduma za Elimu na Utunzaji na Sheria ya Kitaifa ya Huduma za Elimu na Utunzaji, na vile vile Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani inayohusiana na ruzuku za utunzaji wa watoto.
- Usifanye jambo lolote ambalo linaweza kutiliwa shaka haijalishi ni nani atakayekuuliza kufanya hivyo, kwa mfano mzazi kukuuliza utie saini kwamba ulitunza mtoto wao kwa siku ambayo hukufanya hivyo.
- Kumbuka kwamba unawajibikia maamuzi unayofanya. Hakikisha unafanya maamuzi yanayokusaidia kufuata sheria.

Ushauri Bora Zaidi

- Jisajili na huduma ya Family Day Care unayofikiri itakusaidia kuendesha biahsra yako kulingana na sheria na itakayokupa usaidizi na mafunzo unayohitaji.
- Wakati mwingine kuanza na mtoto mmoja au wawili kunaweza kukusaidia kuelewa jinsi utatayarisha nyumba yako na jinsi ya kufanya usimamizi kwa urahisi.
- Fanya mafunzo yote ya kujiunga (kuanza) yanayotolewa na huduma yako.
- Kukosa kujua sheria sio kisingizio cha kuivunja. Kuna sheria nyingi zinazodhibiti kile unachoweza kufanya na usichoweza kufanya kama mwalimu. Jua sheria hizi ni gani.
- Fanya shughuli za usimamizi mapema. Huduma ya Family Day Care inapaswa kukusaidia.
- Hakikisha umetayarisha nyumba yako ili shughuli za kila mara kama vile kubadili winda ziwe rahisi sana iwezekanavyo.
- Fahamu sera na taratibu za huduma yako kwa kusoma na kuangazia mojawapo kila siku. Kufuata sera hurahisisha zaidi kila jambo.
- Hakikisha unapea kipaumbele mahitaji ya watoto kila wakati – hii hurahisisha mambo na hivyo utajua kuwa watoto wanapokea elimu na utunzaji wanaohitaji.

FAHAMU MENGI ZAIDI

Fahamu mengi kwa kutembelea tovuti zifuatazo:

- **www.education.gov.au/compliance**
- **www.fdcsupport.org.au**
- **www.fdca.com.au**
- **www.acecqa.gov.au**

Au kwa kutembelea tovuti ya huduma yako ya Family Day Care au kwa taarifa nyingine yoyote ambayo wametoa kama vile vijitabu vya maelekezo au miongozo ya jinsi ya kuanza.

LAINI YA KUTOA RIPOTI

Iwapo unashuku kuwa kuna ulaghai unaofanyika, unaweza kuwasiliana na Idara ya Elimu na Mafunzo ya Serikali ya Australia kupitia laini yao ya kuripoti na utoe maelezo mahususi kwa 1800 664 231 au utume barua pepe kwa **tipoffline@education.gov.au**

Unaweza kutoa ripoti bila kutaja jina lako iwapo unataka kufanya hivyo..

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.